



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Kumb Na.: BG/DC/E.50/3/VOL.V/69

Tarehe: 24 Septemba, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA UANDIKISHAJI NA UANDAAJI WA ORODHA YA WAPIGA KURA KATIKA VITONGOJI KWA WATUMISHI WA UMMA

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa Mamlaka niliyopewa chini ya Kanuni ya 10(2) na 9(2) ya Kanuni ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji Na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya ya mwaka 2024, Tangazo la Serikali Namba 571 la tarehe 12/7/2024 pamoja na Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka za Miji Midogo ya mwaka 2024, Tangazo la Serikali Namba 572 la tarehe 12/7/2024, Ninapenda kuwatangazia Watumishi wote wa Umma kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya muda ya kuandikisha na kuandaa Orodha ya wapiga kura katika vitongoji kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa mwaka 2024.

SIFA YA MWOMBAJI

- i) Awe Raia wa Tanzania na mwenye umri wa kuanzia miaka 18 au zaidi.
- ii) Awe Mtumishi wa Umma mwenye elimu ya Kidato cha Nne au zaidi na anayejua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
- iii) Awe muadilifu na mwaminifu.
- iv) Asiwe Mtumishi wa Umma katika Kada ya Afisa Mtendaji wa Kata au Mtendaji wa Kijiji.
- v) Asiwe Kiongozi au Kada wa chama chochote cha Siasa.

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz. Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz

MAASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI

- i) Mwombaji lazima aainishe Mtaa anaomba kufanyia kazi.
- ii) Mwombaji lazima aambatishe:-
 - a) Nakala za Vyeti vya Elimu.
 - b) Wasifu Binafsi (CV) unaojitosheleza ukionyesha anwani ya makazi na Namba za simu.
 - c) Picha mbili (2) za 'Passport Size' za hivi karibuni.
- iii) Barua ya maombi ya kazi lazima ipitie kwa mwajiri.
- iv) Barua ya maombi ya kazi itumwe kwa anwani ifuatayo:-

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO,
S. L. P 59
BAGAMOYO.

- v) Maombi ya kazi yatakayoainishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili hayatafanyiwa kazi.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI YA KAZI NI TAREHE 30 SEPTEMBER, 2024



Shauri Selenda
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO.**

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz. Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz